**Learning by Ear 2011 – Mikinzano na utatuzi – "Palipo na wazee"**
Kipindi cha 7: "Ni wakati wetu"
AUTHOR: Chrispin Mwakideu
EDITOR: Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo

## List of characters by scenes:

**SCENE ONE : NINA AND MASAMBO OUTSIDE THEIR HUT**

- **Masambo (m, 50)**
- **Nina (f, 40)**

**SCENE TWO : LAWI AND GULU IN THE OPEN FIELDS WITH CATTLE GRAZING**

- **Lawi (m, 21)**
- **Gulu (m, 17)**

**SCENE THREE: KERO AT MASAMBO'S HUT**

- **Lawi (m, 21)**
- **Kero (f, 55)**
- **Masambo (m, 50)**
- **Nina (f, 40)**

**SCENE FOUR: MITUMBA, SHANI AND LELA PREPARE TO GO OUT**

- **Mitumba (m, 50)**
- **Lela (f, 20)**
- **Shani (f, 17)**

**Msimulizi**

**INTRO:**

Salaam kem kem na karibu katika Noa bongo! Jenga maisha yako. Tumefikia kipindi cha saba katika hadithi ya mizozo na utatuzi, kwa jina, **"Palipo na wazee"**. Katika kipindi kilichopita, tulishuhudia maisha ya amani katika bonde la

AUTHOR: Chrispin Mwakideu
EDITOR: Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo

Kijani baada ya maridhiano. Lakini je, yatadumu? Hususan, baada ya Kero na Somba kumshawishi Rais Matonge awape watu watorube silaha dhidi ya watu wakimbebe. Kumbuka, lengo kuu ni kuzusha rabsha kabla ya uchaguzi. Hili litamaanisha hakuna uchaguzi utakaofanyika katika bonde la Kijani kutakapokuwa kumezagaa tafrani na mapigano. Wacha tuone yatakavyojiri katika kipindi hiki kiitwacho, **"Ni wakati wetu".** Ni asubuhi katika bonde la Kijani, Nina na mumewe Masambo wanakamua ng'ombe wao maziwa nje ya kijumba chao.

## SCENE ONE: NINA AND MASAMBO OUTSIDE THEIR HUT

| |
|---|
| **1. SFX: MORNING AMBIENCE IN THE VILLAGE/cattle sounds** |

**2. MASAMBO:** Nina, unafikiri nilifanya makosa kumuuliza Mitumba kama angependa wasichana wake waolewe na wavulana wetu?

| |
|---|
| **3. SFX: COW BEING MILKED BY HAND INTO A BUCKET** |

**4. NINA:** La, hukukosea katu. Labda, ni vile uliuliza wakati na mahala pasipofaa na kwa watu..

**5. MASAMBO:** **(Cuts her short)** Wakati? Kwani? Nilifikiri ndio wakati sahihi.

**6. NINA:** Watu uliouliza ndio wabaya.

| | |
|---|---|
| **7. MASAMBO:** | Watu wabaya? Nina, si ni wewe na wanawake wengine, muliyekwenda kwa Waliani kumuuliza aje kutupatanisha na watu wa Koroma? Iweje sasa ni watu wabaya kuwaolea watoto wao? |
| **8. NINA:** | Sikusema ni watu wabaya wa Koroma. Usinitie maneno mdomoni, Masambo. Nilichomanisha, kwanza ungeliwauliza hawa wavulana wetu. **(sarcastic)** Pia wao wana kauli yao. Wajua tena. |
| **9. MASAMBO:** | **(sneers)** Wanaweza kuzungumza, hawa wazungumze. Mbona hawajawahi kusema kitu? Lawi anastahili kuwa baba sasa. Nataka kuona wajukuu wangu ati. |
| **10. NINA:** | Unanichekesha. Wajukuu hao watawapata na ng'ombe? Kwa maana siku zote umewapa kazi ya kulisha, kutwa kucha! |
| **11. MASAMBO:** | **(defensive)** Mimi niliweza kuangalia ng'ombe na kukuangalia wewe , na pia wao walipozaliwa. Kama niliweza, mbona wao? |
| **12. NINA:** | Masambo, kama ulifanya yote hayo pekeo, mimi nilikuwa wapi? Eh? |
| **13. MASAMBO:** | **(Hesitant)** Wewe ulikuwa..eh..eh.. |
| **14. NINA:** | Wala sitaki jibu. |

**15. SFX: TRUCK APPROACHING FROM A DISTANCE**

| | |
|---|---|
| **16. NINA:** | Lile ni gari linalokuja? Ni kama linakuja huku! |

17. **MASAMBO:** **(panicking)** Ni waasi waKimbebe! Sasa wamepata gari na wamerudia ng'ombe wangu waliosalia! Haraka Nina, kimbia ndani na ujifiche! Lau sivyo, wanaweza kukuteka nyara kama walivyomteka mke wa Mitumba.
18. **NINA:** **(scared and almost in tears)** Lakini… lakini na wewe Masambo? Je, wakikuua?
19. **MASAMBO:** Nina, usiwe na hofu, hakuna mtu atamuua jasiri kama Masambo! Ingia ndani, wameshafika. Vumbi linaashiria gari liko karibu.

| **20. SFX: COWS MOOING LOUDLY** |
| --- |

21. **MASAMBO:** **(calming himself and the cows)** Ni sawa, ng;ombe wangu..Tulieni..
22. **MSIMULIZI:** Huku Masambo akijipa moyo kuhusu kutoweka kwa ng'ombe wake, Nina alikuwa amejibanza pembeni katika giza ndani ya kijijumba chao, wote wanasubiri majaliwa. Sio mbali na hapo, kule malishoni, Lawi na Gulu walipokua wanalisha ng'ombe wa baba yao, pia waliliona gari , na wakapigwa na butwaa kulikoni bondeni. Kwani ni nadra magari kuja katika bonde la Kijani.

**<u>SCENE TWO: LAWI AND GULU IN THE OPEN FIELDS WITH CATTLE GRAZING</u>**

| **23. SFX: CATTLE GRAZING, MOOING** |
| --- |

24. **GULU:** **(alarmed coughs from the dust in the air)** Lawi!

Umeliona hilo gari?

**25. LAWI:** Ndio nimeliona, Gulu. Linaonekana kama linaelekea kijijini mwetu.

**26. GULU:** Unafikiri wamekuja kwa sababu gani? Sikuliona kwa ajili ya vumbi.

**27. LAWI:** Sijui Gulu, inaweza kuwa mtu yeyote. Labda wanasiasa wanaweza kuwa wamekuja kuomba kura, au wanunuzi wamekuja kununua mali, au wanajeshi wanachunga mipaka. Sina uhakika.

**28. GULU:** Pia wewe utampigia kura Roselyn? Mama alisema atakuwa Rais wa kwanza mwanamke nchini, ni kweli?

**29. LAWI:** **(irritated)** Sijui na sijali!

**30. GULU:** Una shida gani? Umenibadilikia tangu niende kuwasaidia kazi kina Lela na Shani. Hiyo ndiyo sababu umenuna?

**31. LAWI:** **(Angry)** Bado siwezi kujisamehe kwa kupoteza ng'ombe wetu kwa waasi wa Kimbebe. Tulikuwa na mamia ya ng'ombe, sasa tumesalia na hawa wachache. Ni lazima tuwapate! Ni lazima tupate hata zaidi!

**32. GULU:** Lakini Lawi, sikulaumu kwa yaliyotokea. Achana nao!

**33. LAWI:** Hapana! Nilimuahidi baba nitawaregesha, na nitaweka ahadi yangu.

**(Nina, their mother comes in panting)**

**34. NINA:** Lawi! Gulu! Nashukuru nimewapata hapa. Efu!..**(catches breath)**

| | |
|---|---|
| **35. GULU:** | **(concerned)** Mama kumetokea nini? Kila kitu shwari nyumbani? |
| **36. LAWI:** | Shwari kivipi Gulu. Ni lini ulimuona mamako akitimua mbio hadharani jinsi hii? |
| **37. GULU:** | Hakuna. |
| **38. NINA:** | Watoto wangu, baba yenu anawaita. Anawataka nyumbani haraka! |
| **39. LAWI:** | Kuna nini mama? Ndio tumefika na ng'ombe hata hazijakula vyakutosha. |
| **40. NINA:** | Musiniulize mimi mtamuuliza baba yenu. Sasa harakisheni na murudi nyumbani na ng'ombe. Kuna mgeni anawasubiri. |
| **41. GULU:** | Mara mgeni, mara ng'ombe. Kuna harusi yanukia. Lawi anataka kumuoa nani, mama? Lela? |
| **42. NINA:** | **(nervous)** Njooni nyumbani. Huyu mgeni amekuja na masanduku ya mbao, kwanza tulifikiri ni waasi wa Kimbebe wamekuja kuiba ng'ombe, lakini inaonekana ni mtu mkuu serikalini. |
| **43. LAWI:** | Sasa, nimeelewa. Kumbe ni gari la wanajeshi. Njoo, Gulu, tuwaregeshe ng'ombe nyumbani. |
| **44. GULU:** | **(Leads cows)** Huku… Shhh … Njia hii! |

| |
|---|
| **45. SFX: COWS BEING LED BY STICK OR WHIP** |

**46. MSIMULIZI:** Lawi, Gulu na Nina, walianza kurudi na ng'ombe wao nyumbani. Huko walisubiriwa na Masambo baba yao pamoja na Kero

ambaye ni mkuu wa upelelezi nchini. Masambo na Kero walikua wakinywa maziwa huku wakipiga gumzo.

**SCENE THREE: KERO IN MASAMBO'S HUT**

| |
|---|
| **47. SFX: SIPPING OF A DRINK (studio)** |

| | |
|---|---|
| **48. MASAMBO:** | Bw. Kero, nikuongezee maziwa zaidi? Wavulana wangu watafika hapa sasa hivi. |
| **49. KERO:** | Ndio, tafadhali. Haya ni maziwa yana ladha nzuri sana sijawahi kunywa maziwa kama haya! |
| **50. MASAMBO:** | **(proudly)** Hmm, asante bwana. Lakini nijulishe zaidi kuhusu mpango huu wa serikali . |
| **51. KERO:** | Kama nilivyokueleza, kwa muda mrefu tumewaona watorube mkiteseka. Hawa waasi washenzi wakimbebe wamekuwa wakiwasumbua kila wakati. Wanaiba ng'ombe wenu, wanasababisha ukosefu wa usalama na kuleta woga kwa wapenda amani kama nyinyi. Sasa serikali imeamuwa kuwapa watorube wote bunduki na risasi , ili muweze kujilinda. |
| **52. MASAMBO:** | **(curious)** Lakini kwanini sasa, kwanini munatupa bunduki sasa? Baada ya muda wote huo? Binafsi nimepoteza ng'ombe wangu kwa wezi wa ng'ombe. Serikali ilikuwa wapi wakati huo? |
| **53. KERO:** | Bw. Masambo, unahitaji msaada wetu au la? Tayari familia nyengine zimefurahia silaha hizo . Kama utataka kuhatarisha maisha yako ni juu yako. |

**54. MASAMBO:** Sikunuia kukuudhi, Bwana. Bila shaka, ninataka familia yangu na ng'ombe wangu wawe kwenye mazingira salama.

**55. SFX: DOOR BEING KNOCKED**

**56. MASAMBO:** Ah wavulana wangu ndio hawa. Narudi.

**57. SFX: DOOR BEING OPENED**

**58. LAWI:** Baba, hujambo? Tumeharakisha tuwezavyo.

**59. MASAMBO:** Karibuni, tafadhalini msalimieni mgeni wangu. Ana jambo lakutueleza.

**60. KERO:** La, utawaelezea. Vijana, nifuateni garini, nitawaachia mwanajeshi mmoja atakayewafunza jinsi ya kutumia bunduki. Tuna taarifa kuwa wezi wa ng'ombe waKimbebe wamepanga kuiba ng'ombe, na hata kamanda wao, wameenda kuiba ng'ombe. Sasa ni wakati mzuri wa kuvamia.

**61. NINA:** **(shocked)** Bunduki? Bunduki zipi? Masambo, kunaendelea nini?

**62. MASAMBO:** Mumemsikia mgeni. Twendeni nje. Nitawaeleza zaidi baadae.

**63. MSIMULIZI:** Kero aliitembelea familia za waTorube moja baada ya nyengine, ambapo aliwapa bunduki na risasi, na kumbakisha mwanajeshi

wa kuwafunza jinsi ya kuzitumia bunduki hizo. Muda mfupi baada ya kuondoka, utulivu, na mazingira ya amani katika bonde la Kijani uligubikwa na sauti na kelele za risasi. Anga ghafla ikajaa moshi. Wakaazi wote wa bonde la Kijani wakaingia hofu, wakiwemo jamii ya Mitumba, Shani na Lela ambao tayari walikuwa wanajiandaa kwenda shambani..

**SCENE: FOUR: MITUMBA, SHANI AND LELA PREPARE TO GO OUT**

| **64. SFX: SEVERAL GUNS BEING FIRED** |
|---|

**(Lela and Shani screaming in fear)**

**65. SHANI:** **(scared and screaming)** Wuuuuuiiiiii. Baba, saidia!!

**66. LELA:** Tumevamiwa!

**67. MITUMBA:** **(Shouts)** Lela, Shani, rudini ndani! Funga mlango!

| **68. SFX: DOOR BEING CLOSED IN A HURRY** |
|---|

**69. MITUMBA:** Sasa laleni chini! Inamisheni vichwa. Musisimame!

**(Heavy breathing from Lela and Shani)**

**70. LELA:** **(Panicky)** Ni nani? Mbona watulenge risasi?

**71. MITUMBA:** Labda, Labda ni waasi waKimbebe. Wao ndio kundi haramu pekee wenye bunduki.

**72. SHANI:** Lakini … Lakini hatujawakosea na lolote! Mbona watake kutuua?

**73. MITUMBA:** Hata mimi sifahamu. Lakini tutajuwa. Tulieni! Narudi sasa hivi.

**74. SHANI:** **(very scared)** Usitoke nje baba! Tafadhali usiende!

**75. MITUMBA:** Shani kaa chini!

**76. SFX: DOOR SLOWLY BEING OPENED**

**77. LELA:** Baba, tafadhali kuwa muangalifu.

**78. SFX: SEVERAL BULLETS FIRED AGAIN**

**79. MITUMBA:** **(Screams in pain)** Aaaah! Wamenipiga risasi!

**80. SHANI:** **(Shouts)** Baba!!!

**81. LELA:** **(Shouts)** La!!!!!

**OUTRO:**

Na huku vilio vikizagaa katika familia ya Mitumba, tunafikia mwisho wa kipindi hiki cha saba. Je, familia ya Mitumba itanusurika? Ni nani anayewafyatulia risasi? Athari yakuwapa watorube silaha itakua ipi? Kwa majibu ya haya maswali, usikose kipindi kifuatacho cha **"Palipo na wazee".** Kama unataka kusikiliza tena kipindi hiki, au vipindi vingine vilivyotangulia, tembelea tovuti yetu **www.dw.de/kiswahili**

Hadi tutakapokutana tena, kwaheri.